## KUNDI B: SARE ZA SHULE.

**SARE YA DARASANI.**

- **i.** Sketi mbili (**02**) rangi ya **zambarau** zenye rinda box la upana wa inchi nane na urefu wa sketi uwe sentimita ishirini 20 tokea usawa wa goti la mwanafunzi kuelekea chini. **WAISLAMU** sketi iwe ndefu kabisa hadi miguuni**.** (**muhimu sana**)
- **ii.** Shati mbili nyeupe za mikono mifupi, na Kwa waislamu shati mbili za mikono mirefu **(HALF KANZU HAZIRUHUSIWI)**
- **iii.** Sweta moja rangi ya zambarau (**ifanane na rangi ya sketi**)
- **iv.** Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba, (**mashimo ya kamba kuanzia manne kila upande**) kisigino kifupi na visiwe na mapambo yoyote. (Mabuti, travota, viatu vingine vyenye mapambo na viatu vilivyo na matundu ya kamba pungufu ya manne**, HAVIRUHUSIWI KAMA SARE YA SHULE**)
- **v.** Aje na soksi rangi nyeupe **ndefu** (stocking socks) jozi mbili
- **vi.** Tai ndefu rangi ya zambararu.

**SARE YA KUSHINDIA.**

- i. Sketi mbili nyeusi zenye rinda box la upana wa inchi nane na urefu wa sketi uwe sentimita ishirini 20 tokea usawa wa goti la mwanafunzi kuelekea chini. **WAISLAMU** sketi iwe ndefu kabisa hadi miguuni**.** na t shirt mbili (02) nyekudu **round collar** zisizo na maandishi, **-** sare hii ni **kwa ajili ya kushindia**.
- ii. Kwa waislamu **hijabu** za kushindia na "*vya kuvalia ndani ya hijabu*" ni rangi **nyeupe tu**, zisizo na urembo wowote. **Hijabu iwe ndefu inayofunika mikono yote.** Atavaa awapo darasani na hata katika sare ya kushindia.
- **iii.** Aje na track suti rangi ya bluu kwa ajili ya kuvaa wakati wa kujisomea usiku.

**SARE ZA MICHEZO.**

- **i.** Kila mwanafunzi aje na bukta na tshirt rangi ya light blue (jezi ya Manchester city) raba nyeupe kwa ajili ya michezo.

**KUNDI C: Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:**

1. Madaftari makubwa (counter book) ya kutosha masomo yake, mazoezi na majaribio.
2. Ream ya karatasi **(A4) -** mbili (2) kwa mwaka
3. Kalamu za kutosha za wino, penseli, ufutio, stapler mashine na stapler pins.
4. Scientific Calculator.
5. **Dissecting kit** kwa mwanafunzi anayesoma somo la Baiolojia.
6. Vitabu vya masomo kwa tahasusi husika. (**vimeorodheshwa uk. wa 06**)
7. Godoro la inchi $2^{1}/_{2}$ x 6, Shuka 2 za rangi ya pinki, Chandarua, Ndoo ndogo ya kuogea, Sanduku dogo la chuma, (asije na begi la nguo sanduku la chuma yaani tranka linatosha.) Mto na foronya, Torch na betri,
8. Vyombo vya chakula, bakuli (container) kijiko na kikombe.

**VIFAA VYA USAFI –** viletwe kwa mgawanyo ufuataao:-

| KWA WANAFUNZI WA HGL | VIFAA KWA WANAFUNZI WA CBG |
|---|---|
| - Ndoo kubwa ya lita 20<br>- Squizer moja<br>- Dawa za chooni lita tano (**05 ltrs**) | - Jembe lenye mpini moja.<br>- Ndoo kubwa ya lita 20<br>- Squizer moja<br>- Ufagio wa chelewa wenye kishikio cha mti.<br>- Mfagio wa buibui. |

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZILIZOTAJWA JUU KABISA**

Pia Ndugu mzazi/mlezi unashauriwa umfungulie mwanao akaunti ya benki itakayokuwezesha wewe kumtumia mwanao pesa ya matumizi madogo madogo awapo shuleni. Huduma za benki zipo karibu na shule bila usumbufu wowote. Huduma za Benki zilizopo karibu na shule ni pamoja na **NMB, CRDB, MKOMBOZI BANK** na **EQUITY BANK.**
**"Shule haitahusika na upotevu wa pesa yoyote itakayotumwa kwenye namba yoyote ya simu.**

